



# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS,  
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA



## HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO

Kumb: Na. AB.113/388/01/75

Tarehe: 01 Agosti, 2024

### TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo amepokea Kibali cha Ajira Mbadala kutoka kwa Katibu Mkuu OR - Utumishi chenye **Kumb.Na. FA. 228/613/01/D/040** ya tarehe **09.07.2024**. Hivyo anapenda kuwatangazia Watanzania wote wenye sifa kutuma maombi kwa kada moja (1) kama ilivyoainishwa kwa kuzingatia sifa tajwa hapo chini: -

#### 1.0 MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU DARAJA LA II – NAFASI 1

##### 1.1 MAJUKUMU YA KAZI

- i. Kuorodhesha barua zinzoingia masjala kwenye rejista (incoming correspondence register);
- ii. Kuorodhesha barua zinazotoka nje ya taasisi kwenye rejista (outgoing correspondence register);
- iii. Kusambaza majalada kwa watendaji (action officers);
- iv. Kupokea majalada yanayorudi masijala toka kwa watendaji;
- v. Kutafuta kumbukumbu/nyaraka/majalada yanayohitajika na watendaji;
- vi. Kurudisha majalada kwenye shubaka/kabati la majalada (racks/filling cabinets) au mahali pengine yanapohifadhiwa
- vii. Kufuatilia mzunguko wa majalada ndani ya Taasisi (file tracking)

##### 1.1.1 SIFA ZA MWOMBAJI

Awe Muhitimu wa Kidato cha Nne au Sita mwenye Stashahada au NTA level 6 ya Utunzaji wa Kumbukumbu kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali, mwenye ujuzi wa Kompyuta.

##### 1.1.2 NGAZI YA MSHAHARA

Kwa kuzingatia Ngazi za Mishahara ya Serikali -TGS C.

## **MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI**

- i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenyе umri kuanzia miaka 18 – 45
- ii. Waombaji wote waambatanishe nakala ya cheti cha kuzaliwa.
- iii. Barua ya muombaji ioneshe anuani anayotumia kwasasa pamoja na namba ya simu ikiambatana na:-
- iv. Nakala za vyeti vya taaluma.
- v. Nakala ya vyeti vilivyothibitishwa na Mwanasheria/Wakili ambavyo ni vyeti vya kidato cha nne, sita na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa na kazi husika.
- vi. Maelezo binafsi yanayo jitoshaleza (Detailed CV) yenye anuani na namba za simu zinazopatikana na majina ya wadhamini (Referees) watatu wa kuaminika.
- vii. Picha mbili (2) za “**Passport Size**” za hivi karibuni.
- viii. Kitambulisho cha Taifa au namba ya Kitambulisho cha Taifa (**NIDA**)
- ix. Waombaji waliowahi kupatikana na kosa la jinai hawatafikiriwa
- x. “**Testmonies**”, “**Provisional Result**”, “**Statement of Results**” hati ya matokeo ya Kidato cha nne na sita (**FORM IV AND FORM VI RESULT SLIPS HAVITAKUBALIWA**).
- xi. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU, NECTA na NACTE).
- xii. Waombaji waliostaafishwa/kuachishwa kazi katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama ana kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.
- xiii. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi, wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.
- xiv. Waombaji wenye sifa zaidi ya zilizotajwa hapo juu maombi yao hayatafikiriwa.
- xv. Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni **tarehe 09 Agosti, 2024**.

- xvi. **MUHIMU:** Kumbuka kuambatisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya elimu, anuani ya barua hiyo ielekezwe kwa;

**Mkurugenzi wa Manispaa,  
Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo,  
S.L.P 55068,  
DAR ES SALAAM.**

- xvii. Maombi yote yatumwe kwenye Mfumo wa Kielektroniki wa Ajira (Recruitment Portal) kuitia anuani ifuatayo; <https://portal.ajira.go.tz/> (Anuani hii pia inapatikana kwenye tovuti ya Sekretarieti ya Ajira kwa kuingia sehemu ilioandikwa "Recruitment Portal".
- xviii. Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioanishwa katika tangazo hili **HAYATAFIKIRIWA.**

Tangazo hili limetolewa na;

Aron T. Kagurumjuli  
**MKURUGENZI WA MANISPAA**

---

**Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi wa Manispaa. Luguruni, Barabara ya Morogoro, S.LP: 55068, Dar es Salaam, Unaweza pia kuwasiliana nasi kwa Simu. 0222-926341, Nukushi: 0222-92342, Tovuti; www. ubungomc.go.tz, Barua pepe; info@ubungomc.go.tz**

